TODAYSKY COMPANY LIMITED
P.O BOX 1552 Dodoma

website: www.2daysky.com
Email: huduma@2daysky.com
Phone: +255 693 157 658
Meriwa road

# MWONGOZO WA KUTUMIA MFUMO WA SkyStock

## UTANGULIZI

Karibu katika mfumo wa SkyStock. SkyStock ni mfumo wa Kidigitali ambao unarahisisha usimamizi wa biashara au miradi mbalimbali. Mfumo huu kwa sasa unakuwezesha kufanya yafuatayo:-

1.Kusimamia biashara/miradi mbalimbali ndani ya mfumo mmoja

2.Kutunza taarifa za mauzo katika biashara/miradi

3.Kutengeneza ankra(Invoice) za kulipia cash na kukopesha

4.Kutunza taarifa za wateja waliohudumiwa

5.Kusajili bidhaa zote

6.kuingiza stock iliyopo stoo, iwapo stock itaisha unaweza kuongeza stock mpya.

7.Kuhifadhi kumbukumbu za matumizi katika biashara mfano malipo ya kodi ya pango, umeme, nk

8.Kupata ripoti za mauzo ya kila siku kwa njia ya barua pepe.

9.Kupata ripoti ya mauzo ya siku, wiki, mwezi na mwaka mzima

10.Kutunza kumbukumbu ya malipo ya wafanyakazi

11.Uwepo wa kutoa ofa na punguzo kwa wateja katika misimu mbalimbali, mfano msimu wa sikukuu wa mwaka mpya.

12.Kusimamia wafanyakazi, uwezo wa kuongeza wafanyakazi kwenye mradi kulingana na kazi anayoifanya, mfano store manager, msimaizi wa mauzo nk.

SkyStock inapatikana katika Muundo wa tovuti : [https://stock.2daysky.com/](https://stock.2daysky.com/) , ukifungua linki hii utakutana na ukurasa wa nyumbani kama unavyoonekana hapo chini,





*Ukurasa wa nyumbani*

## SEHEMU YA KWANZA (01)


1. Kujisajili Na Kuingia Katika Mfumo Wa SkyStock

   Kama ni mtumiaji wa mara ya kwanza; Bofya sehemu iliyoandikwa **SAJILI** au tengeneza akaunti, na ukurasa wa kuweka taarifa binafsi utafunguka, weka majina kamili, namba ya simu, barua pepe na nywila kisha bofya **ENDELE**. Taarifa binafsi ni za muhimu kwa ajili ya kulinda akaunti yako.




*Ukurasa wa kujisajili*

Kama ni mtumiaji ambaye tayari una akaunti ya SkyStock, Bofya sehemu iliyoandikwa **INGIA** na ukurasa wa kuweka hati tambulishi(Username na password) utafunguka, weka barua pepe au namba ya simu na nywila(Password), kisha bofya **INGIA.**





*Ukurasa wa kuingia(Login)*

Ikiwa hati tambulishi (Username na password) ni sahihi basi ukurasa wa sehemu ya pili utafunguka.

**SEHEMU YA PILI( 02 )**

## 1. Fungua Mradi Mpya


Bofya sehemu iliyoandikwa **FUNGUA MRADI MPYA,** kisha jaza taarifa kuhusu mradi/biashara husika kama vile : Jina la mradi, anuani ya mradi na namba ya simu kwa mradi husika(namba ya simu unaweza kutumia namba ambayo huwa unatumia kuwasiliana na wateja wako, au namba binafsi), alafu bofya **TUMA** kusajili mradi/biashara.




*Ukurasa wa kutengeneza miradi*

## 2. Tazama Miradi

Kutazama au kuingia kwenye biashara/miradi iliyosajiliwa bofya sehemu ya **MIRADI ILIYOPO.**




### 3. Lipia Akaunti / Vifurushi vya SkyStock

Jaribio la kutumia mfumo kwa mradi uliosajiliwa, litafanyika ndani ya siku saba (7), na baada ya hapo mtumiaji anatakiwa kuchangia kiasi fulani kulingana na vifurushi au akaunti, ili kuendelea kutumia huduma hiyo.


**Kifurushi cha Tarangire**, Mtumiaji atalipia sh. 5,000 ili kuwa na uwezo wa kutengeneza mradi mmoja ambao atautumia kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya kufanya malipo tena.

**Kifurushi cha Ngorongoro,** mtumiaji atalipia sh. 10,000 ili kupata uwezo wa kutengeneza na kusimamia biashara au Miradi mitatu ambayo pia ataitumia ndani ya mwezi mmoja kabla ya kufanya malipo tena.

Kifurushi cha Serengeti, mtumiaji atalipia sh. 15,000 ili kupata uwezo wa kutengeneza na kusimamia miradi bila kikomo, atatumia kifurushi hiki kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya kufanya malipo tena.

Malipo katika vifurushi yanaweza kufanyika kadri ya mahitaji ya mteja, yanaweza kuwa kwa mwezi, miezi mitatu, miezi sita au mwaka mzima.

Malipo yote yatafanyika kupitia M-Pesa, Tigo Pesa au Airtel Money. Namba ya Kampuni: **767676,** Namba ya kumbukumbu: **252** ikifuatiwa na namba ya simu unayotumia kwenye akaunti yako ya SkyStock.




*ukurasa wa kuingia kwenye mradi*

## SEHEMU YA TATU ( 03 ): Namna ya kuingia kwenye mradi

Bofya **INGIA** ili kuanza kutumia SkyStock kwenye mradi husika. Baada ya kuingia utakutana na sehemu(link) zifuatazo:


### 1. Link ya Nyumbani

Sehemu hii inaonyesha Mauzo ya taarifa za mauzo katika biashara/mradi, taarifa hizi ni za mauzo ya siku, wiki na mwezi, pia sehemu hii inaonyesha bidhaa zinazokaribia kuisha pamoja na

matumizi mengine yanaweza kufanyika mfano manunuzi ya umeme, bili za maji, chakula nk.


## 2. Weka stock Mpya Katika Mradi.

Bofya sehemu iliyo andikwa **STOCK,** kisha chagua **WEKA STOCK MPYA**, na sehemu ya kusajili bidhaa katika mradi, pamoja na sehemu ya kuongeza stock zitafunguka. Hatua hii ni ya awali kabla ya kuanza kufanya mauzo, hivyo ni lazima kufanya usajili wa bidhaa kwanza pamoja na kuweka stoo yako kwenye mfumo.




## 3. Sajili Bidhaa.


Sajili bidhaa zilizopo kwenye biashara/mradi kwa kuandika jina la bidhaa, jina la kipimo cha jumla mfano katoni, kreti, box, gharama ya kuuza bidhaa kwa bei ya jumla, jina la kipimo cha rejereje mfano chupa, pisi,kipande nk, gharama ya kuuza bidhaa kwa bei ya rejareja, idadi ya bidhaa inayounda jumla mfano idadi inayounda jumla ya kreti la soda ni 24, kisha bofya **TUMA.**




*Ukurasa wa kusajili bidhaa*

## 4. Ongeza Stock.


Chagua moja ya bidhaa zilizo sajiliwa, kisha weka idadi ya bidhaa zilizopo kwenye stoo ya duka/mradi pamoja na zilizotumika kununua bidhaa husika, kisha bofya **TUMA**, ili kuongeza stock katika mradi.




*Ukurasa wa kuongeza stoo(stock)*

### 5. Tazama Stock / Bidhaa Katika Mradi.

Bofya sehemu ya taarifa za stock kujua bidhaa zilizopo stoo, na Bofya sehemu ya bidhaa zilizosajiliwa kuona bidhaa zilizosajiliwa katika mradi.





Bofya hapa kuangalia bidhaa zilizopo stoo

Bofya hapa kuona bidhaa zilizosajiliwa


## 6. Tengeneza Invoice / Ankara

Ili kuanza kuingiza taarifa za mauzo bofya sehemu iliyoandikwa **TENGENEZA INVOICE**, ili kupata ukurasa wa kuingiza bidhaa zilizouzwa,

Weka tarehe ya invoice / ankara, jina la mteja, namba ya simu na anuani kisha bofya TUMA, Baada ya kutuma ukurasa wa kuweka bidhaa katika ankara / invoice itafunguka, kisha chagua bidhaa,weka bidhaa kwa jumla na rejareja kama ipo, alafu bofya neno **TUMA,**





Bofya hapa kuingiza taarifa za mauzo




*Ukurasa wa kuuza bidhaa*


## Tanzama  invoice / ankara

Bofya sehemu iliyoandikwa Taarifa za Invoice kisha  chagua invoice zilizolipwa kujua taarifa za ankara zilizokwishalipwa na mteja au chagua invoice (Mkopo), kujua taarifa za invoice ambazo hazijalipwa, tumia sehemu kufanyia kazi invoice za mteja baada ya kufanya malipo ya mkopo wake.





## Tazama Ripoti

Bofya sehemu iliyoandikwa **REPORT** ili kupata taarifa zote za mauzo, unaweza kupata taarifa za tarehe husika, tarehe fulani hadi tarehe fulani,



### Weka Matumizi Ya Ziada.


Bofya sehemu iliyoandikwa MATUMIZI MENGINE, kisha chagua WEKA MATUMIZI AU LIPA MISHAHARA, ili kuingiza taarifa za matumizi katika mradi wako, mfano malipo ya umeme, bili za maji na chakula.




*Ukurasa wa kuweka matumizi mengine*

### Simamia Wafanyakazi

Ili kuweza kuongeza wafanyakazi au wasimamizi wengine wa biashara au mradi bofya sehemu iliyoandikwa **MIPANGILIO**, kisha changua **WAFANYAKAZI,** ukurasa wa kuingiza taarifa za mfanyakazi/msimamizi utafunguka.






*Ukurasa wa kuongeza wafanyakazi*

## Simamia Akaunti

Ili kuweza kufanya mabadiliko ya taarifa za mradi au biashara husika, Bofya sehemu iliyoandikwa **MIPANGILIO**, kisha chagua **AKAUNTI** ili kupata ukurasa wa kuhariri Mradi.

Bofya Linki ya akaunti kuhariri




*Ukurasa wa kuhariri taarifa za mradi*